# GRADE 7 MID TERM 2 MAY 2022

# KISWAHILI

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako**

***Ikamilishe insha hii kwa maneno yako huku ukiifanya ya kusisimua zaidi.***

*Haikuwa kawaida yangu kutembea usiku. Siku hiyo.........................................*

# TARGETER WINGS DARASA LA SABA - MWAKA 2022

## MTIHANI WA MJARABU

## KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA

**Wings 002**

***MUDA: Saa 1 dakika 40***

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Ukitaka kuwa bora maishani lazima kama___1__ ujiboreshe.___2__ ukitaka kuwa duni basi___3___. Ubora hutafutwa vilevile uduni. Lakini kujiboresha hadi uwe bora kunahitaji___4___na kujitolea sana. Ni kujituma__5__ ili kuepuka hali ya kubakia duni au ovyo.__6___tusisahau kwamba mtu akiwa na nia ya kuwa bora maishani hazubai,___7___, hujitahidi kutafuta mbinu na njia___8___ kumpigisha hatua hadi awe bora. Husemwa___9___. Nacho kinolewacho hupata.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** ibada | **B.** mauti | **C.** sheria | **D.** desturi |
| **2.** | **A.** Licha ya | **B.** Wala | **C.** Aidha | **D.** Mbali na |
| **3.** | **A.** jidumishe | **B.** jidunishe | **C.** jidunishiwe | **D.** jidumishiwe |
| **4.** | **A.** uzembe zaidi | **B.** ugoigoi zaidi | **C.** utepetevu kidogo | **D.** bidii zaidi |
| **5.** | **A.** kufa kuzikana | **B.** kufa kupona | **C.** kula kubakisha | **D.** kutia na kutoa |
| **6.** | **A.** Ila | **B.** Ili | **C.** Pia | **D.** Aidha |
| **7.** | **A.** hakati tamaa | **B.** haendi nguu | **C.** husumbua riziki | **D.** havunji miko |
| **8.** | **A.** yote ya | **B.** zote ya | **C.** zote za | **D.** zozote ya |

**9.** **A.** pang'okapo jino pana pengo **B.** nazi mbovu harabu ya nzima
**C.** kanga hazai ugenini **D.** jembe halimtupi mtu

Mambo mengi huwapata watu maishani lakini Mungu hufufua nyama kitangani. Kwa __10__ maisha yetu yalikuwa mazito na magumu. Umaskini ulikita hema kwetu. Ninakumbuka tulikula makombo maponeo na vyakula___11__ _12__. Tulivaa mademu kwa maana ya matambara. Tulilala katika kibanda___13__ cha udongo na karatasi___14___watoto na wazazi wetu wawili, baba na mama. Umaskini wetu ulituvaa kama joho nasi tukashindwa__15__ kuuvua. Kwa kweli mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | **A.** yamkini | **B.** hakika | **C.** huenda | **D.** yawezekana |
| **11.** | **A.** tulivyoviokota | **B.** tulizookota | **C.** tuliokota | **D.** tutazookota |
| **12.** | **A.** dukani | **B.** hotelini | **C.** jaani | **D.** sokoni |
| **13.** | **A.** mbovu | **B.** mbaya | **C.** kibovu | **D.** chafu |
| **14.** | **A.** nyinyi nyote | **B.** wao wote | **C.** sisi wote | **D.** sisi sote |
| **15.** | **A.** vile ya | **B.** jinsi ya | **C.** namna ya | **D.** hata |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Tumia 'ndi' kwa usahihi
Chai hii ________ tamu zaidi
A. ndiyo B. ndio
C. ndizo D. ndilo

**17.** Maneno haya ni
Haa!, Zii!, Hewala!Usu!
A. Vihusishi B. vielezi
C. sifa D. viingizi

**18.** Zama na Zeina ni ndugu wa tumbo moja yaani ni ndugu wa
A. kufa kuzikana B. toka nitoke
C. tui na maziwa D. leo na kesho.

**19.** Chagua sentensi iliyotumia kielezi cha mahali.
A. Usihusudu kufanya uhalifu wowote daima.
B. Jogoo aliwika mara tatu leo.
C. Mahafali ya kufuzu kwa shahasa ya uzamili yatafanywa mwakani.
D. Visu vyote vikali viwekwe kabatini.

**20.** Ni sentensi gani iliyonyambuliwa katika kauli ya kufanyiza
A. Wanachuo walirushiwa mayai viza.
B. Mwalimu Bakari hunifundishia watoto vizuri.
C. Watoto wa jamii tofauti huingiliana vyema wanapocheza.
D. Tulifunganya virago vyetu tukatorokea msituni.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**21.** Upi ni usemi wa taarifa wa:
*"Simamisha gari hili papa mara moja," afisa wa trafiki alitoa amri.*
A. Afisa wa trafiki aliamrisha gari hilo lisimamishwe pale mara moja.
B. Afisa wa trafiki aliagiza gari lisimamishwe mara moja.
C. Afisa wa trafiki aliomba gari lisimamishwe hapo mara moja.
D. Afisa wa trafiki aliamrisha gari hilo lisimamishwe hapa mara moja.

**22.** Neno "aliwatahadharisha" lina silabi ngapi?
A. 15 B. 17
C. 8 D. 9

**23.** Ni kitu kipi kinachopatikana baharini pekee?
A. shaba B. lulu
C. dhahabu D. almasi.

**24.** Ipi ni ushuri mbili?
A. $^1/_{12}$ B. $^2/_{10}$
C. $^2/_8$ D. $^3/_9$

**25.** Zari alikuwa ameshikilia mboga zilizokuwa zimefungwa pamoja. Yaani Zari alikuwa ameshikilia
A. bunda la mboga B. kitita cha mboga
C. fungu la mboga D. kicha cha mboga

**26.** Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti huitwaje?
A. Tarbia. B. Takhmisa.
C. Tasdisa. D. Tathlitha.

**27.** Tabia yake ya wizi ilimfanya anyongwe kwa kamba, yaani
A. ale kalenda
B. aweke nadhiri
C. atiwe kitanzi
D. ale kiapo.

**28.** Tamko litumiwalo na watu ili kuwafariji waliofikwa na msiba wa kifo ni
A. makiwa B. simile
C. pole D. samahani.

**29.** Ni methali gani iliyo na maana ya: Fimbo ya mbali haiui nyoka
A. Dua la kuku halimpati mwewe.
B. Kivuli cha fimbo hakimfichi mtu jua.
C. Moto hauzai moto.
D. Ulingo kwa kwae haulindi Manda.

**30.** Kasa ________ majini haning'inii.
Tumia kiambishi sahihi kujazia nafasi.
A. ya B. wa
C. za D. la

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Siku za punde joto limeongezeka kwa kiasi kikubwa si barani tu bali pia duniani kote. Ongezeko hili limezidi kupuuzwa japo athari zake ni dhahiri. Fahamu kinaganaga kuwa joto hilo limezidi kutokana na shughuli za wanadamu wenyewe. Kiwango cha gesi ya kabonidioksidi na methani kimezidi hewani. Gesi hizo hutokana na kuvuta sigara, vichemuo vya magari moshi kutoka viwandani na kemikali zinazonyunyiziwa mimea. Gesi hizi zinaendelea kuathiri na kuharibu tabaka la Ozoni, tabaka ambalo ni murua inayokinga miali hatari ya jua kutufikia duniani. Kwa hivyo, miali hatari ya jua imeanza kutufikia na kusababisha ongezeko la joto duniani.

Athari yake kubwa ni kuongezeka kwa jangwa. Sehemu kame inazidi kuongezeka na wanasayansi wanasema kwamba iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa, huenda dunia yote ikawa jangwa katika nusu karne ijayo. Haya ni madai ambayo yameanza kudhihirika katika sehemu nyingi za ulimwengu. Athari zake ni pamoja na upungufu wa chakula duniani kwa sababu asilimia tisini ya vyakula vyetu hutokana na mimea. Hata vyakula vinavyotokana na wanyama pia vinazidi kupungua kwa sababu wanyama hula mimea.

Vilevile, joto jingi linaloshuhudiwa linayeyusha theluji iliyopo vileleni pa milima na sehemu za kaskazini na kusini mwa dunia. Maji hayo yaliyoyeyuka huingia baharini na itakuwa ni hatari mno endapo theluji yote itayeyuka kwani dunia yote itageuka na kuwa bahari maadamu theluji iliyopo duniani ni nyingi mno. Hili linadhihirika pale ambapo visima vingi vimeanza kumezwa na maji kutokana na ongezeko la maji baharini. Watu wameshurutishwa kuhamia kwingine kwa sababu makazi yao yamesombwa na maji.

Matumaini ya kuzidi kuwepo kwa nchi zilizotokana na juhudi za binadamu kunyakua ardhi inayopakana na bahari kama vile nchi ya Uholanzi katika karne ijayo kutategemea sana kiwango cha joto duniani. Ukitaka kuona athari hii hapa petu, unahitaji kutembelea miji iliyoko ukingoni mwa bahari Hindi kama vile Mombasa, Dar es Salaam, Malindi na Lamu. Maji yameanza kuongezeka upya na mawimbi yenyewe yanakuwa mazito sana licha ya kwamba yanaleta mchanga mwingi sana ufuoni.

Hoteli nyingi za kitalii zilizo pwani zimepata matatizo sana kwani maji haya huenea hadi kutoka hoteli hizo. Nyingi zimejenga kuta za kukingana na mawimbi ya bahari lakini mara kwa mara, maji huvunja kuta hizo na kuujaza mchanga kwenye mandhari maridadi ya hoteli hizo. Hali hiyo inasababisha bughudha katika sehemu hizo za kifahari ambako watalii huja kupunga unyunyu.

31. Kwa mujibu wa aya ya kwanza, ni sahihi kusema kuwa
A. joto limeanza kutokea duniani siku za hivi karibuni
B. watu wengine nchini ndio wanaopuuza athari za joto duniani
C. gesi inayoathiri ukanda wa ozoni ni oksijeni.
D. miale athari ya jua itaanza kutufikia kwa muda mfupi ujao.

32. Ni shughuli gani kati ya zifuatazo haichafui mazingira?
A. Kuzuia mmomonyoko wa udongo.
B. Moshi wa viwandani.
C. Kunyunyizia mimea dawa.
D. Vichemuo vya magari barabarani.

33. Umuhimu wa tabaka la ozoni ni
A. huyakinga mazingira kutokana na uchafuzi
B. husafisha gesi chafu
C. huzuia miale hatari ya jua kufika duniani
D. hukinga miale ya jua kufika duniani.

34. Kwa mujibu wa wanasayansi, dunia huenda ikawa jangwa baada ya karibu miaka mingapi endapo hatua za haraka hazitachukuliwa?
A. 100 B. 50
C. 1000 D. 500

35. Athari ya kwanza ya jangwa ni
A. kupungua kwa maji baharini
B. kuongezeka kwa maji baharini
C. vifo vya wanyama na wanadamu
D. ukosefu wa chakula cha binadamu na wanyama.

36. Kwa mujibu wa taarifa, ni kipi ambacho husababisha ongezeko la maji baharini?
A. Joto linaloyeyusha theluji kwenye sehemu za kasikazini, kusini na milimani.
B. Jangwa linaloyeyusha theluji ya milimani.
C. Joto jingi linaloyeyusha theluji ya milimani.
D. Joto jingi duniani.

37. Taarifa imeonyesha mfano gani wa nchi ambayo huenda itasombwa na maji na inapatikana bara gani?
A. Uholanzi - Afrika.
B. Uholanzi - Amerika.
C. Uholanzi - Uropa.
D. Uholanzi - Asia.

38. Athari ya ongezeko la maji baharini unaweza kuonekana upwa wa Afrika Mashariki ni
A. ongezeko la joto jingi upwani
B. ongezeko la maji mengi na mchanga upwani
C. hoteli nyingi kufungwa
D. kuyeyuka kwa theluji ya visiwa vya pwani.

39. Kupunga unyunyu ni sawa na
A. kujivinjari
B. kutalii
C. kwenda mandhari
D. kutembea kwa miguu.

40. Kwa mujibu wa taarifa, ni nani ana suluhisho la ongezeko la joto duniani?
A. Mungu.
B. Mwanadamu.
C. Wanasayansi.
D. Tabaka la ozoni.

***__Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.__***

Maisha yangu ya utotoni hadi sasa nikiwa wa miaka zaidi ya miongo mitatu hayajakuwa papai kwa kijiko. Nilipokopolewa, mambo yalikuwa ndivyo sivyo, yalikuwa magumu ajabu. Licha ya hiyo, wazazi wangu walitunukiwa utajiri wa busara na hekima. Baba yangu alikuwa mtu mwenye mkono wazi na roho safi kwani wengi wa wanakijiji walimsaka kwa kuauniwa kwa hili ama lile. Wengi wa waliofika kwetu walihitaji mawaidha naye hakuwavunja nyoyo zao bali aliwatimizia haja zao bila swali wala shari.

Wazazi wangu walinilea vyema, mama akinitimizia mahitaji ya chakula na mavazi naye abu akinitimizia mahitaji ya karo na ***marudi***. Nami kama wasemavyo, niliwalanda wazazi wangu kwa hulka na sura. Husemwa, tunda bovu lawama kwa mti.

Mawaidha ya baba yangu yalikuwa zaidi ya kurunzi ya kunimulikia baadaye. Nami sikujaribu kumvunja moyo bali nilizifuata nyoyo zake. Elimu waliyonipa ilikuwa ni ya kuridhisha tu kwani ***__sikufua dafu__*** kuzidi kiwango cha msingi kutokana na uchechefu wa karo. Hayo yaliendelea hata wanuna wangu nao hawakuangukiwa na nyota ya jaha kuzidi darasa la nane.

Kaka yangu mlungizi alikuwa mtambuzi wa mambo na mchapakazi. Huko shuleni hakuliwazia sana ukosefu wa kwetu bali alizidisha bidii maradufu. Mtihani wa mwisho wa masomo ya darasa la nane ulipofika, hakulaza damu, bali alijipinda mgongo sawasawa na hatimaye matokeo yake yakawafurahisha na hata kuwavuta wahisani walioyadhamini masomo yake. Aliendelea kufanya vyema na baada ya masomo ya chuo kikuu, aligura huko jijini alikopata gange ya donge nono. Hakutukumbuka ngo.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Huku nyumbani mambo yalizidi kuwa yale yale. Nilihitimu miaka ya kufunga pingu za maisha na kwa hi yo nikawaendea wazazi wangu kuwataka ridhaa ilivyokuwa desturi ya watu wa jamii yetu. Bila shaka w linikubalia. Saka saka ilianza na hatimaye nikampata barafu ya moyo wangu.

Sherehe ya harusi iliandaliwa kwa hisani ya wanakijiji. Wao ndio waliojitolea kugharamia kila kitu kilichohitajika shereheni. Mahari niliyotoa yalitolewa na wazazi wangu. Ng'ombe mmoja, mbuzi mmoja na kuku wawili. Wakwe zangu walikubali na kusema bora amani katika ndoa.

***Mke wangu alikuwa malaika aliyetumwa na Maulana***. Aliniomba nimtafutie shilingi elfu tano tu hata kama ningekopesha. Alizitumia hizo na kuanzisha biashara ya kuuza mavulia. Hizi ni nguo zilizovaliwa na wengine maarufu kama mitumba, "baada ya miezi mitano, alikuwa amezirudisha pesa hizo alizozitumia kuanzisha biashara pamoja na riba yake. Leo hii kutokana na biashara yake, tumeanza kuitwa watu. Kaka mlungizi aliporejelea nyumbani kuja kujenga aliachama. Kwetu kulikuwa peponi. Ama kweli Mungu si Athmani.

41. Mwandishi anamaanisha nini anaposema maisha yake hayakuwa papai kwa kijiko?
    A. Maisha yake yamekuwa ya raha mustarehe.
    B. Maisha yake yote yamekuwa yenye mateso na mashaka.
    C. Maisha yake hayajakuwa rahisi.
    D. Maisha yake yamekuwa mchafukoge.
42. "Mungu hamnyimi mtu vyote" methali hii imedhihirikaje?
    A. Licha ya wazazi wake mwandishi kuwa maskini wa mali, walikuwa matajiri wa busara na hekima.
    B. Ingawa kwao mwandishi walikuwa maskini, yeye alikuwa mwerevu na akasoma sana kuliko ndugu zake.
    C. Watu waliipenda familia ya mwandishi licha ya kuwa walikuwa maskini.
    D. Familia yake mwandishi ilikuwa maskini na tajiri wa watoto.
43. Watu wengi walifika kwa mwandishi kwa nia ya
    A. kusaidiwa chakula
    B. kuelimishiwa wanao
    C. kutatuliwa matatizo yao
    D. kusaidiwa kulipiwa karo.
44. Ni maelezo yapi yasiyo sahihi kulingana na ufahamu?
    A. Wazazi wa mwandishi walikuwa watu karimu.
    B. Mama alishughulikia afya na lishe.
    C. Msomaji aliwalanda wazazi wake kwani naye alikuwa mshauri kwa wengine.
    D. Mwandishi alilelewa kwa hulka akhyari na uwajibikaji.
45. Neno <u>marudi</u> limetumiwa katika ufahamu. Lina maana ya
    A. mateso B. mapenzi
    C. manung'uniko D. maonyo.
46. Ni maelezo yapi sahihi kwa mujibu wa ufahamu?
    A. Watoto wote walisoma na kukamilisha masomo yao ya shule ya upili.
    B. Ndugu zake mwandishi hawakumaliza masomo yao.
    C. Watoto wote wa familia hii walikuwa samaki.
    D. Si nduguze wote waliokosa elimu ya maana.
47. Maneno ***sikufua dafu*** inamaana kuwa
    A. sikufaulu
    B. sikushindwa
    C. sikuelewa
    D. sikumaliza
48. ***Kazi ya donge nono*** ni kazi ya aina gani?
    A. Kazi ngumu.
    B. Kazi ya hadhi.
    C. Kazi ya sulubu.
    D. Kazi ya kulazimishwa.
49. "Mke wangu alikuwa malaika aliyetumwa na maulana " Nukuu hii imetumia tamathali gani ya lugha?
    A. Tashihisi. B. Tashibihi.
    C. Sitiari. D. Nahau.
50. Ni maelezo gani yasiyo sahihi kulingana na aya ya mwisho?
    A. Mkewe mwandishi hakuwa wa kawaida kwani alitumwa na Mungu.
    B. Nguo ziiizovaliwa na wengine huitwa mavulia.
    C. Mwandishi alibahatika kupata mke mchapakazi.
    D. Ukikifanyia kitu chochote bidii, bila kuenda nguu, utafaulu.